# CHAMA CHA WAFANYAKAZI WA TAASISI YA ELIMU YA JUU, SAYANSI, TEKNOLOJIA, HABARI NA UTAFITI (RAAWU)

# SERA YA JINSIA NA MAENDELEO YA WANAWAKE WA RAAWU

TOLEO LA MWAKA 2009

CHAMA CHA WAFANYAKAZI WA TAASISI YA ELIMU YA JUU, SAYANSI, TEKNOLOJIA, HABARI NA UTAFITI (RAAWU)

# SERA YA JINSIA NA MAENDELEO YA WANAWAKE WA RAAWU

TOLEO LA MWAKA 2009

# Yaliyomo


Dibaji ..... iii
Msamiati tafsiri, na vifupisho ..... v

1.0 UTANGULIZI ..... 1

2.0 LENGO LA SERA ..... 2
- 2.1 Shabaha/Madhumuni ya Sera ..... 2

3.0 DHANA YA JINSIA ..... 3

4.0 HISTORIA YA MASUALA YA JINSIA–RAAWU ..... 4
- 4.1 Mafanikio ..... 4
- 4.2 Matatizo ..... 6
- 4.3 Elimu ..... 6
- 4.4 Majukumu ya kifamilia ..... 6
- 4.5 Mtazamo hasi ..... 6
- 4.6 Ujuzi na Maarifa ..... 6
- 4.7 Idadi ya wanachama wanawake ..... 7

5.0 HALI YA WANAWAKE KATIKA AJIRA ..... 7

6.0 MATAMKO YA SERA NA MIKAKATI YA UTEKELEZAJI ..... 8
- 6.1 Usawa na Jinsia ..... 8
- 6.2 Utekelezaji nafasi za Uongozi kwa wanawake ..... 8
- 6.3 Ushiriki wa wanawake katika shughuli za Chama ..... 8
- 6.4 Elimu ya Vyama vya Wafanyakazi kwa Wanawake ..... 8
- 6.5 Bughudha za kijinsia kwa wanawake ..... 9
- 6.6 Mahusiano na wadau mbalimbali ..... 9
- 6.7 Nafasi za Ajira kwa wanawake ..... 9
- 6.8 Uwekaji wa kumbukumbu na takwimu ..... 10
- 6.9 Kamati za Wanawake ..... 10
- 6.10 Habari na Mawasiliano ..... 10
- 6.11 Uratibu wa masuala ya jinsia ..... 11
- 6.12 Mifuko ya Hifadhi ya Jamii ..... 11
- 6.13 Wanawake na Mazingira ..... 11
- 6.14 Wingi na uzito wa kazi kwa wanawake ..... 12
- 6.15 Afya ya wanawake na uzazi ..... 12
- 6.16 Mapambano dhidi ya VVU na UKIMWI ..... 13
- 6.17 Ushirikishwaji wa wanawake ..... 14

6.18 Haki za wanawake .......... 14

7.0 USIMAMIZI NA TATHMINI .......... 14

# SERA YA JINSIA NA MAENDELEO YA WANAWAKE

## DIBAJI

RAAWU inaamini katika usawa wa jinsia. Katika kuthibitisha imani hii, Katiba ya RAAWU kuanzia toleo la mwaka 2000, 2005 na toleo la mwaka 2009 katika ibara ya Kumi (10) imeweka bayana muundo unaoonyesha namna masuala ya wanachama wanawake yatakavyoshughulikiwa katika ngazi zote za chama, yaani, Tawi, Kanda na Taifa. Uamuzi huu wa Chama wa kuingiza masuala ya wanawake kwenye Katiba umesaidia sana kuinua ushiriki wao kwenye shughuli za Chama.

Wengi wametambua, kwa mfano kwa kuhudhuria kwenye vikao au mikutano ya Chama na kutoa michango yao, na kugombea nafasi mbalimbali za uongozi wa Chama ni haki na wajibu wao. RAAWU imeandaa sera hii, kwa kuzingatia msimamo wa serikali katika kuinua hali za wanawake kwa kuhimiza upangaji na utekelezaji mipango unaozingatia ushirikishwaji wa wanawake na wanaume kwa uwiano ulio sawa na unaokubalika na wote. Aidha, sera hii itazingatia masuala ya msingi yaliyobainishwa kwenye sera ya Shirikisho la Vyama vya Wafanyakazi Tanzania (TUCTA).

Ili kurahisisha na kuwezesha utekelezaji wa dhana ya Jinsia, Sera imeelekeza na kuhimiza uimarishwaji wa Kamati za wanawake katika ngazi zote za Chama na kuwepo kwa kitengo maalumu kikachohusika na uratibu wa masuala ya wanawake ndani ya Chama.

Kufanikiwa katika utekelezaji wa masuala ya wanawake kutategemea sana msukumo wa vyombo vikuu vya Chama hususan, Halmashauri za matawi na Kamati za Utendaji za Kanda na Taifa, katika kuwezesha kusimamia na kufuatilia mipango ya Kamati za Wanawake na utekelezaji wake na kutoa ushauri wa mara kwa mara unaolenga kuinua ushiriki sawa wa wanaume na wanawake katika shughuli za Chama.

Napenda kutoa shukrani za dhati kwa Kamati ya Utendaji ya Taifa kwa kutoa maelekezo ya kuandaliwa kwa sera hii. Aidha, napenda kutoa shukrani kwa wajumbe wa Kamati za Utendaji Kanda na Taifa ambao mchango wao wa maoni na ushauri umesaidia kwenye kuandaa sera hii, bila kuisahau sekretarieti ya Makao Makuu ambayo ilihakiki kwa makini yaliyomo kwenye sera hii.

**(VIII) UKANDAMIZAJI**

Ni utumiaji wa nguvu za madaraka ili kudumisha utawala dhalimu kijinsia, ambao unawafaidia wale wanaotawala, kwa madhara ya wale wanaotawaliwa. Kwa hiyo ukandamizaji wa wanawake humaanisha utawala unaotumika kudumisha udharaulishi na kumnyima mwanamke haki sawa na mwanaume katika jamii.

**(IX) USAWA WA KIJINSIA**

Hali ya kutokuwa na ubaguzi kwa misingi ya jinsia ya mtu katika mgao wa rasilimali au mapato, au katika ufikiaji wa huduma mbalimbali za kijamii. Usawa wa kijinsia unaweza kupimika kwa mifano ya kuwepo kwa fursa sawa au matokeo sawa.

**(X) U K U W A**

Kifupi cha maneno ***"Usawa wa Kijinsia na Uwezeshaji wa Wanawake".***

**(XI) USHIRIKISHWAJI**

Unatafsiriwa kuwa hali ya wanawake kushiriki kwa idadi sawa na wanaume katika harakati za maendeleo. Hapa tunazingatia usawa katika kushiriki kufanya maamuzi.

| | | |
|---|---|---|
| (XII) | **RAAWU** - | (Researchers Academicians & Allied Workers Union |
| (XIII) | **TUCTA** - | Trade Union Congress of Tanzania |
| (XIV) | **OTTU** - | Organization of Tanzania Trade Union |
| (XV) | **JUWATA** - | Jumuiya ya Wafanyakazi Tanzania |
| (XVI) | **PSI** - | Public Service International |
| (XVII) | **GAD** - | Gender and Development |
| (XVIII) | **VVU** - | Virusi vya UKIMWI |
| (XIX) | **UKIMWI** - | Upungufu wa kinga mwilini |
| (XX) | **CEDAW** - | Convention on Elimination of all Forms of Discrimintion Against Women. |

### 4.7 Idadi ya wanachama wanawake

Idadi ya wanawake walioajiriwa kwenye Taasisi wanachama wa RAAWU ni theluthi moja (⅓) ya wanachama wote wa RAAWU. Hali hii imechangia sana kuwa na uwakilishi mdogo wa wanawake kwenye nafasi za uongozi na katika shughuli nyingine za Chama.

## 5.0 HALI YA WANAWAKE KATIKA AJIRA

Kutokana na msimamo wa Taifa baada ya uhuru kuhusu usawa na haki za binadamu, sheria za kazi zilizokuwa na ubaguzi zilifanyiwa marekebisho. Hii ni pamoja na sheria ya ajira **Sura 360** na sheria ya mishahara na marupurupu **Sura 300** ambazo zilielekeza mwanaume kulipwa zaidi ya mwanamke hata pale wanapokuwa na sifa zinazolingana. Sheria na taratibu za nchi haziruhusu kuajiri kwa kuangalia jinsi bali sifa na uwezo wa waombaji wa kazi.

Aidha kwa Taasisi za Umma, suala la ujira haliangalii mwanaume au mwanamke. Wote wanapewa mshahara sawa kulingana na kazi wanazofanya.

Kwa Taasisi za binafsi ni aghalabu pia kuona ubaguzi wa wazi kwenye ajira na ujira.

Hata hivyo yapo mazingira ambayo ni vigumu kubaini ubaguzi, hasa pale mwajiri anapokuwa na dhamira binafsi.

Licha ya kuwepo kwa sheria kali, dhidi ya vitendo vya unyanyasaji kwa wanawake, bado hali hiyo ipo; inayomhusisha mwajiri au wafanyakazi wenyewe kwa wenyewe.

Chambuzi mbalimbali zinaonesha kuwa suala la haki, ukombozi wa wanawake na usawa wa kijinsia, uwezeshaji wa wanawake, kuongeza nguvu, uwezo na mabadiliko ya wanawake wafanyakazi siyo suala la wanawake pekee bali suala la jamii nzima. RAAWU iitike katika kuchukua hatua madhubuti ili kujenga dunia mbadala ya wafanyakazi, kuhakikisha wanawake na wanaume wana haki na fursa sawa kwa manufaa ya wote.

## 6.0 MATAMKO YA SERA NA MIKAKATI YA UTEKELEZAJI

### 6.1 Usawa wa Kijinsia

**Tamko:** RAAWU inaamini kuwa wanachama wote ni sawa na wana haki sawa katika kushiriki shughuli zote za Chama.

**Mkakati:** RAAWU itaendeleza na kusimamia ushiriki wa wanawake katika nafasi za utekelezaji.

### 6.2 Nafasi za Uongozi kwa wanawake

**Tamko:** Mwanachama yeyote wa RAAWU awe mwanaume au mwanamke mwenye kutimiza masharti yote ya uanachama ana haki ya kugombea nafasi yoyote ile ya uongozi katika Chama.

- Katika kipindi hiki cha kuhamasisha ushiriki wa wanawake, RAAWU itaendelea kutekeleza mpango wa kutenga nafasi maalumu za uongozi kwa ajili ya wanawake kuanzia ngazi ya tawi hadi Taifa kwa utaratibu utakaoonekana unafaa ili mradi katika vyombo vyote vya Chama vya kikatiba uwakilishi wa wanawake usiwe chini ya asilimia thelathini (30%).

  **Mkakati:** Wanawake watahamasishwa kugombea nafasi mbalimbali za kimaamuzi za Chama.

### 6.3 Ushirikishwaji wa wanawake

Hali ya ushirikishwaji wa wanawake RAAWU katika kufikiwa kwa maamuzi mbalimbali ya Chama sio mbaya sana kutokana na mfumo uliopo wa Kamati ya Wanawake. Mfumo huu unatoa fursa kwa wanawake kuwa na uwakilishi katika vyombo vyote vya Chama na katika ngazi zote. Hata hivyo lengo ili kufikia asilimia hamsini (50%) bado halijatimia.

### 6.4 Elimu ya Vyama vya Wafanyakazi kwa wanawake

**Tamko:**

Chama kitaandaa mpango maalumu wa kutoa elimu ya Vyama vya Wafanyakazi kwa wanachama wanawake. Lengo ni kuwaongezea uwezo, kuwapa kujiamini na kufanya shughuli za Chama kwa ufanisi zaidi. Kwa namna hiyo imani ya wanachama kwa wanawake itaongezeka na hivyo kupewa nafasi zaidi za uongozi na uwakilishi.



Wafanyakazi ni ya wanaume. Ndio wanaoiweza na sio wanawake. Lakini hatimaye walianza kubadilika na kuwa na mtazamo tofauti. Ndio maana RAAWU haikuona jambo la ajabu kumchagua Bibi Adelgunda Mgaya kuwa Naibu Katibu Mkuu wa kwanza mwanamke kwenye Chama hicho na alikuwa mwanamke pekee aliyepata nafasi ya Naibu Katibu Mkuu wakati Vyama huru vya Wafanyakazi vinaanzishwa nchini kati ya mwaka 1993 – 1995.

RAAWU ilikuwa miongoni mwa Vyama vichache vya Wafanyakazi vilivyoitikia wito wa PSI wa kuundwa kwa Kamati za Wanawake kama hatua ya kutekeleza Mpango kusudio "Affirmative Action" wa kuongeza ushirikishwaji wa wanawake.

Licha ya kuwa suala la Kamati za Wanawake lilikuwa halijaingizwa kwenye Katiba ya Chama, uamuzi wa pamoja ulifikiwa kwenye vikao vya Kitaifa vya Chama, kuwa Mwenyekiti na Katibu wa Kamati ya Wanawake katika ngazi zote wawe wanaingia kwenye vikao vya kikatiba vya Chama.

Mwaka 2000 wakati wa marekebisho ya Katiba ya RAAWU suala la Kamati za Wanawake liliingizwa rasmi kwenye Katiba na kuboreshwa zaidi kwenye marekebisho ya mwaka 2005 na 2009.

Hatua ya kuingiza masuala ya Kamati za Wanawake kwenye Katiba ilisaidia sana kuongeza uwakilishi wa wanawake kwenye vikao vya kikatiba vya Chama.

Kamati za Wanawake ziliweza kuhamasisha wanawake wafanyakazi wakajiunga na Chama na kujitokeza kwenye kugombea nafasi mbalimbali za uongozi.

Katika Uchaguzi Mkuu wa mwaka 2000 ngazi ya Kanda na Taifa wanawake wapatao 700 walijitokeza kugombea nafasi mbalimbali za uongozi na kati yao 38 waliweza kushinda.

Katika Uchaguzi Mkuu wa 2005 wanawake waliojitokeza kugombea ni 1005 Kati yao 59 waliweza kushinda.

Hivyo hadi kufikia mwaka 2005 uwakilishi wa wanawake kwenye nafasi za uongozi kuanzia ngazi za Tawi hadi Taifa ulifikia asilimia 22 kutoka asilimia 12 ya mwaka 1995.

## 4.2 Matatizo

Licha ya mafanikio yanayoelezwa, yalikuwepo matatizo kadhaa ya msingi ambayo yalirudisha nyuma juhudi za Chama za kuinua ushiriki wa wanawake. Bado hatujafikia mapinduzi ya kuridhisha katika kujenga mahusiano ya haki na usawa wa kijinsia. Bado kuna pingamizi nyingi zinazozuia ufikiaji wa hali ya juu ya ukombozi wa wanawake, haki na usawa wa kijinsia katika ngazi na maeneo yote ya maendeleo na maisha ya wafanyakazi wanawake matatizo ni pamoja na yafuatayo:-

## 4.3 Elimu

Idadi kubwa ya wanawake walioajiriwa kwenye Taasisi zinazowakilishwa na RAAWU wana elimu ya chini na wachache elimu ya kati na juu. Kwa hali hiyo, wengi walikosa ujasiri na kutojiamini na hivyo kushindwa kushiriki kwenye kugombea nafasi za uongozi. Kwa wanawake inabidi kuzingatia kutoa elimu katika mazingira ya kusoma na kuweka mikakati inayotoa nafasi zaidi kwa wanawake kusoma.

## 4.4 Majukumu ya kifamilia

Wanawake wengi walisita kugombea nafasi za uongozi na hata kushiriki mikutano kutokana na majukumu ya kifamilia.

## 4.5 Mtazamo hasi

Kutokana na fikra zilizojengeka miongoni mwa wanaume, na wanawake kwamba kazi ya uongozi ni ya wanaume, hali hiyo ilichangia sana kwa wanawake kutojitokeza au kuchaguliwa kushika nafasi za uongozi. Kushamiri kwa mtizamo na fikra za mfumo dume ni tatizo la msingi linaloendeleza unyanyasaji wa kijinsia na upendeleo kwa wanaume.

## 4.6 Ujuzi na Maarifa

Kugombea na kushinda nafasi ya uongozi kunahitaji sana uwezo pekee wa mgombea katika; kujieleza, kushawishi, kuendesha kampeni, na kudhihirisha uwezo wake kulingana na kazi za Chama alizowahi kufanya. Wanawake wengi hawajapata elimu ya kutosha ya masuala ya Vyama vya Wafanyakazi (Trade Unionism). Mbinu za kuhutubia, kuendesha kampeni na ushawishi.



- Kutoa tafsiri sahihi ya dhana ya jinsia na wanawake katika maendeleo ya Chama na kuhakikisha maendeleo ya jamii kwa ujumla.
- Kusimamia utekelezaji wa matamko ya Kitaifa na Kimataifa kuhusu jinsia.
- Kufafanua dhana ya jinsia na maendeleo (GAD) na utekelezaji wake.
- Kuingiza masuala ya wanawake katika mkondo mkuu wa Chama (Gender mainsteaming).
- Kuhamasisha na kushirikisha waajiri kuhusu dhana ya jinsia.
- Kubainisha mahusiano yaliyopo baina ya RAAWU, Serikali, waajiri, asasi zisizokuwa za kiserikali, TUCTA na Vyama vyake Shiriki na jamii katika suala zima la Jinsia na Maendeleo.
- Kuweka mfumo endelevu wa kushughulikia masuala ya jinsia katika Chama.

## 3.0 DHANA YA JINSIA

Tanzania ni nchi inayothamini usawa na haki za binadamu. Imani hii imeelezwa katika Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya Mwaka 1977 kama ilivyorekebishwa Mwaka 1984. Katiba inasisitiza usawa na heshima kwa binadamu wote, heshima ya kutambua na kuthamini utu wa mtu pamoja na kuhakikisha haki mbele ya sheria.

Katika kifungu cha tatu Katiba ya nchi inalinda uhuru wa mtu mwanaume au mwanamke kupata hifadhi ya maisha, kumiliki mali na pato la jasho lake, kufanya kazi na kupata haki ya kujielimisha kufikia upeo wake. Katiba inafungamana na kuwepo kwa jamii yenye usawa, haki, uhuru na fursa sawa kwa watu wote kuweza kushiriki na kutumia kwa ukamilifu uwezo na vipaji walivyonavyo katika shughuli za Umma, Uongozi, Utamaduni, Uzalishaji mali na Upatikanaji wa huduma na kuwa na hali bora zaidi ya maisha na Taifa.

Kutokana na imani hiyo Tanzania imekwishatia saini Tamko la Umoja wa Mataifa kuwa binadamu wote ni sawa na wana haki sawa mbele ya sheria na katika kugawiwa raslimali au huduma mbali mbali za jamii Aidha Tanzania imetia saini mkataba wa nchi huru za Afrika unaotambua haki za binadamu wote, vile vile imeridhia Mkataba wa Umoja wa Mataifa wa kuondoa aina zote za Ubaguzi na uonevu kwa wanawake.

RAAWU Kama mojawapo ya Taasisi za jamii yenye wanaume na wanawake inapaswa kuwa mstari wa mbele katika kuheshimu na kutekeleza kwa Vitendo msimamo wa Taifa na matamko au mikataba ya kimataifa kuhusu wanawake.

Ni Vigumu kuelezea dhana hii bila ya kuhusisha neno "jinsi". Jinsi; ni maumbile ya wanawake na wanaume. Majukumu ya wanawake yatokanayo na jinsi zao ni kuzaa na kunyonyesha watoto wakati wanaume wakiwa na majukumu tofauti na hayo. Dhana ya jinsia ni mahusiano kati ya wanawake na wanaume yaliyojengwa na yanayoendelea kujengwa na jamii, kutokana na tofauti zao za kimaumbile – mgawanyo wa majukumu ya kazi, mgawanyo wa mapato na raslimali nyingine fursa sawa kushiriki katika siasa na utawala, mila na desturi mbalimbali.

Dhana ya jinsia inalenga katika kuleta usawa kati ya wanaume na wanawake katika maeneo yote yanayohusu haki, amani na maendeleo ya kiuchumi, kijamii, kiutamaduni na kisiasa.

## 4.0 HISTORIA YA MASUALA YA JINSIA KATIKA RAAWU

### 4.1 Mafanikio

Wakati RAAWU inaundwa mwezi Novemba mwaka 1994, tayari ulikwisha kuwepo mwamko wa kutosha miongoni mwa wajumbe kuhusu haki za wanawake. Mwamko huo ulitokana na juhudi kubwa iliyofanywa na OTTU kupitia Kurugenzi yake ya Maendeleo ya Wanawake na Vijana. Aliyekuwa kiongozi wa Kurugenzi hiyo Bibi Halima Kasungu alitoa mchango wa pekee katika kujenga ufahamu kwa jamii ya wafanyakazi kuhusu haki za wanawake. Haikuwa kazi rahisi kutokana na ukweli kwamba wengi wa viongozi waliokuwa OTTU na ambao walitokea pia JUWATA walikuwa na fikra kuwa kazi ya kuongoza Vyama vya



## 1.0 UTANGULIZI

Dhamira ya RAAWU ni kuona kwamba wanachama wanawake wanashiriki kikamilifu kwenye shughuli zote za Chama sambamba na wanaume

Hatua kadhaa zimechukuliwa na Chama kwa lengo la kuinua ushiriki wa wanawake. Hatua hizi ni pamoja na; utekelezaji wa dhana ya "nafasi za upendeleo" ambayo ilielekeza wanawake kuhusishwa kwenye programu zote za Chama. Kuanzishwa kwa Kitengo maalumu cha kuratibu masuala ya jinsia na kuingizwa kwa masuala ya jinsia katika Katiba ya Chama ambapo kumesaidia sana kuweka mfumo wa kushughulikia masuala ya jinsia katika ngazi zote za Chama.

Theluthi moja ya wanachama wa RAAWU ni wanawake. Idadi hii ndogo imetokana na mfumo ambao haukutilia maanani suala la jinsia na uendelezaji wa mwanamke.

Kutokana na utayari wa kisiasa na nia thabiti ya Serikali ya kumkomboa mwanamke na kutokana na juhudi za umoja wa wanawake nchini, Vyama visivyo vya kiserikali na wanaharakati mbalimbali, na pia msukumo wa kidunia, suala la jinsia limepata msukumo mkubwa ambao kwa kiasi kikubwa umebadili mtazamo wa jamii kuhusu wanawake.

Hivi sasa wanawake wanapata nafasi za elimu sawa na wanaume kama mojawapo ya hatua ya utekelezaji wa sera ya Taifa kuhusu kumwinua mwanamke.

Nafasi za ajira na hususan Serikalini na kwenye mashirika ya Umma zimekuwa zikitolewa kwa kuzingatia falsafa ya "fursa sawa kwa wote".

Yapo matumaini makubwa kwamba kutokana na mwamko uliopo hivi sasa idadi ya wanawake watakaoingia kwenye ajira itaongezeka maradufu na kwa hivyo kuongezeka pia kwa wanachama wanawake.

Katika kipindi chote cha uhai wa RAAWU, masuala ya wanawake yamekuwa yakishughulikiwa kwa maelekezo ya Katiba ambayo

yamejikita zaidi kwenye uundwaji na utendaji wa Kamati za Wanawake katika ngazi zote za Chama yaani Matawi, Kanda na Taifa.

Shirikisho la Kimataifa la Vyama vya Wafanyakazi wa sekta ya huduma kwa Umma (PSI), limetoa mchango mkubwa sana katika kuhamasisha na kuimarisha harakati za masuala ya wanawake kwa Vyama vyake Shiriki ikiwemo RAAWU.

Kukamilika kwa sera hii na kuwepo kwa utekelezaji makini kutasaidia sana kuharakisha kufikiwa kwa malengo ya kuingiza masuala ya jinsia kwenye mkondo mkuu wa Chama (Gender mainstreaming).

Kwa kuwa tayari ipo sera ya Taifa ya maendeleo ya wanawake na jinsia, ambayo inawahusu wanawake wote nchini, na kwa kuwa Shirikisho la Vyama vya Wafanyakazi Tanzania (TUCTA) linayo sera yake ya jinsia inayowalenga wanawake wote walioko kwenye ajira, sera hii ya RAAWU itatekelezwa kwa kuzingatia yaliyomo kwenye sera ya Shirikisho.

## 2.0 LENGO LA SERA

Kuwa na Chama ambacho wanawake na wanaume wanapewa fursa sawa katika shughuli zote za uendeshaji wa Chama. Bila ya ubaguzi wa aina yoyote ile, kulingana na sifa na uwezo wa kila mmoja.

## 2.1 MADHUMUNI YA SERA

Madhumuni ya sera ya jinsia na maendeleo ya wanawake ni:

- Kutoa mwelekeo utakaohakikisha kuwa mipango mikakati na shughuli mbali mbali za uongozi na uendeshaji wa Chama zinazingatia usawa wa kijinsia.

- Kuweka bayana majukumu ya wanawake na wanaume ili wote waweze kushiriki kikamilifu katika shughuli za maendeleo ya Chama na jamii.

**Utekelezaji:** Kuhakikisha wanawake wanahudhuria semina na programu mbalimbali za elimu.

### 6.5 Bughudha za kijinsia kwa wanawake

- **Tamko:** Chama kitachukua hatua kali za kisheria dhidi ya mwajiri, au mfanyakazi yeyote atakayefanya kitendo cha udhalilishaji kwa mfanyakazi mwenzake awe mwanamke au mwanaume.

- Wanawake watahamasishwa kujitokeza na kuonyesha maovu na udhalilishwaji wanaofanyiwa.

### 6.6 Mahusiano na wadau mbalimbali

- **Tamko:** RAAWU itashirikiana kwa karibu na Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania,Waajiri, Shirikisho (TUCTA), Vyama Shiriki, na Asasi nyingine zisizokuwa za kiserikali katika kuandaa na kutekeleza sera za jumla za masuala ya jinsia na maendeleo ya wanawake nchini.

- RAAWU itaunga mkono kwa hali na mali harakati zozote zile zinazolenga katika kutetea haki na usawa wa jinsia na maendeleo kwa wanawake.

  **Mkakati:** RAAWU itatoa mapendekezo ya mara kwa mara kwa Serikali kuhusu marekebisho ya sheria na sera zinazohusu jinsia au kutungwa kwa sheria zitakazolinda maslahi ya wafanyakazi wanawake nchini.

### 6.7 Nafasi za Ajira kwa wanawake

**Mkakati:** Wakati wa kuajiri wafanyakazi wa kada mbalimbali RAAWU itazingatia jinsia na pale itakapobidi kutoa kipaumbele kwa wanawake kwa lengo la kuwainua na kuwa mfano kwa Asasi nyingine. Lengo ni uwiano usiopungua 1:3 Wanawake watahamasishwa na kuhimizwa kuchukua fursa za ajira zinapojitokeza.

- **Tamko:** RAAWU itaendelea kuhimiza serikali na waajiri katika kutoa fursa sawa kwa wote kwenye zoezi la kuajiri. Hii ni pamoja na kushinikiza kuwepo kwa nafasi maalumu za ajira zitakazotengwa kwa ajili ya wanawake.

**6.8 Uwekaji wa kumbukumbu na takwimu**

- **Tamko:** RAAWU itakusanya kumbukumbu zote zinazoonesha harakati za ukombozi wa wanawake nchini na duniani na kuzihifadhi kwa manufaa ya vizazi vijavyo.

- Kumbukumbu na takwimu zote muhimu za masuala ya jinsia na wanawake zitatunzwa kwenye mtandao kwa minajili ya kuzihifadhi.

- **Mkakati:** Kuwepo na mfumo wa kudumu wa ukusanyaji wa takwimu toka matawini na asasi zingine na kuhifadhi kumbukumbu hizo.

**6.9 Kamati za Wanawake**

- **Tamko:** RAAWU itaendeleza na kuimarisha mfumo wa Kamati za wanawake uliopo hivi sasa na itafanya tathmini ya mara kwa mara kuhusu utendaji wake.

- **Mkakati:** Chama kuendelea kuzitambua Kamati hizo na kuziunga mkono.

**6.10 Habari na Mawasiliano.**

Kupanuka kwa teknolojia ya habari na mawasiliano kumetoa fursa kwa wanawake na wanaume kupata taarifa za kila aina na kwa haraka. Hata hivyo mapungufu ni mengi na juhudi za makusudi zinahitajika ili kupunguza tofauti za ufikiaji wa habari hasa kwa wanawake.

**Tamko:** RAAWU itashirikiana na Asasi nyingine katika kubadilishana taarifa, kuzichambua na kuziwasilisha kwa walengwa kwa wakati muafaka.

**Mkakati:** RAAWU itaandaa vipeperushi na machapisho mbalimbali yanayoelezea dhana ya jinsia na mwelekeo wa Chama kuhusu wanawake angalau mara mbili kwa mwaka, na kuhamasisha wanachama kusoma maandiko hayo.

**Tamko:** RAAWU itashirikiana na Asasi nyingine katika kubadilishana taarifa, kuzichambua na kuziwasilisha kwa walengwa kwa wakati muafaka.



**Mkakati:** RAAWU itatumia njia zozote za habari na mawasiliano zitakazoonekana zinafaa kufikisha ujumbe kwa walengwa.

- **Mkakati:** RAAWU itaweka mfumo maalumu wa utoaji wa habari kwa wanawake, matawini wa masuala yote muhimu yanayowahusu.

**6.11 Uratibu wa masuala ya jinsia na wanawake.**

**Tamko:** Chama kitaendelea kuimarisha uratibu wa masuala ya jinsia na wanawake.

- **Mkakati:** RAAWU itakuwa na ofisi Makao Makuu itakayohusika na uratibu wa shughuli zote za wanawake na jinsia katika Chama.

- Kamati za Wanawake, Tawi, Kanda na Taifa zitatumika kama chachu ya kuhakiki na kuratibu masuala ya kijinsia.

**6.12. Mifuko ya Hifadhi ya Jamii**

Mifuko ya Hifadhi ya Jamii iliyopo nchini haijaweka bayana manufaa ya mifuko hiyo kwa wanawake kama kundi maalumu.

- **Tamko:** RAAWU itaihimiza serikali juu ya kutungwa kwa sheria bora za hifadhi ya jamii zinazolenga kutoa kipaumbele kwa mwanamke hasa katika suala zima la Uzazi na Malezi ya Mtoto hadi atakapomaliza elimu ya sekondari.

- **Utekelezaji:** Kuhamasisha wanachama kuhusu Mifuko ya Hifadhi ya Jamii na kupokea maoni yao ili kuboresha mifuko hiyo kwa lengo la kukidhi mahitaji.

**6.13 Wanawake na Mazingira.**

- **Tamko:** RAAWU itaendelea kuunga mkono kampeni na shughuli zozote zile za wanachama na wanawake zinazolenga kuboresha na kuhifadhi mazingira.

- Aidha itashiriki katika kuhimiza Wataalamu wa mazingira kutumia utaalamu wao katika kuimarisha na kulinda mazingira.

- **Mkakati:** Kuwahamasisha wanawake kushiriki katika shughuli zozote zinazohusiana na mazingira.

## 6.14 Wingi na uzito wa kazi kwa wanawake

Imethibitika kuwa wanawake wanashindwa kushiriki shughuli za Chama kikamilifu kutokana na kutingwa na majukumu mengi ya kifamilia.

- **Utekelezaji:** RAAWU itahamasisha kuanzishwa kwa Sera ya Taifa ambapo itashiriki na kuunga mkono,juhudi zozote zile za kuhamasisha jamii kuhusu kuwapunguzia wanawake uzito wa kazi. Hii ni pamoja na kuhimiza utengenezaji na matumizi ya teknolojia rahisi zinazopatikana hapa nchini.

- Kuimarisha huduma za jamii, vituo vya kulea watoto na huduma za afya sehemu za kazi.

- Kuhimiza jamii ili wanaume na wanawake wagawane majukumu kwa haki na usawa na si kuelemea mtu mmoja.

- Kupinga mfumo dume unaopingana na maendeleo ambayo ni ya kijinsia.

- **Mkakati:** Kuendeleza uhamasishaji wa jamii ya wafanyakazi kuhusu haki na usawa wa kijinsia.

## 6.15 Afya na wanawake na uzazi

Wanawake wako katika hatari kubwa zaidi ya kuambukizwa magonjwa yatokanayo na kazi kuliko wanaume. Hii ni kutokana na ukweli kuwa kazi nyingi zilizoko kwenye mazingira machafu kama vile usafi wa vyoo, ofisi, maabara, kufagia barabara, kutunza wagonjwa, bustani n.k. zinafanywa na wanawake.

Aidha wanawake wako katika hatari ya kubakwa na kuambukizwa magonjwa ya zinaa ukiwemo VVU/UKIMWI. Wanawake wenye umri kati ya miaka 20 na 29 wanapata maambukizi ukilinganisha na wanaume ambao ni wale wenye umri kati ya miaka 40 na 44.

Uzazi umeonekana kama jambo la kutisha. Zipo taarifa kuwa wanawake wengi wafanyakazi wamekuwa waoga kuzaa na wengine



wamejiwekea kikomo cha watoto. Yote hayo ni kutokana na afya za wanawake kuwa duni kwa maradhi na ukosefu wa lishe bora, lakini pia vitisho kutoka kwa waajiri wasiotaka mwanamke aendelee kuzaa kwa vile inaathiri nguvu kazi yao. Ni asilimia 46 (46%) tu ya wanawake ambao wanapata huduma ya kujifungua hospitalini na kuhudumiwa na wakunga wataalamu.

Wanawake hawapati muda wa kutosha wa kupumzika baada ya kujifungua, halikadhalika muda wa kunyonyesha.

- Mkakati: RAAWU itashiriki/kuunga mkono mipango ya kitaifa ili kulinda afya ya mwanamke.

- RAAWU itaandaa mpango wa elimu kwa wanachama juu ya Afya na Uzazi Salama.

- RAAWU itahimiza kuboresha Mifuko ya Hifadhi ya Jamii kuhusiana na Afya.

- RAAWU itahimiza kuona kuwa waajiri wanazingatia utekelezaji wa Sheria ya Mifuko ya Hifadhi ya Jamii.

## 6.16 Mapambano dhidi ya VVU na UKIMWI

Utafiti unaonesha kuwa wanawake ndio wanaoathirika zaidi na janga hatari la VVU/UKIMWI. Zipo sababu nyingi zinazotolewa ikiwa ni pamoja na maumbile, kutokuwa na maamuzi kwenye tendo la ndoa na mwenzi wake, kubakwa na umaskini.

- **Tamko:** RAAWU itashiriki kwa vitendo katika kupiga vita UKIMWI. Hii ni pamoja na kuunga mkono kwa vitendo mikakati ya Serikali na Asasi nyingine zilizoko kwenye mapambano dhidi ya UKIMWI.

- **Mkakati:** RAAWU itatilia mkazo suala la elimu kwa njia ya semina, makongomano, mafunzo na stadi kuhusu VVU/ UKIMWI na kuhakikisha kuwepo kwa sera za UKIMWI mahali pa kazi.

### 6.17 Ushirikishwaji wa wanawake

**Tamko:** RAAWU itahakikisha kuwa ushiriki wa wanawake katika vikao vya **maamuzi** unapanuliwa na kufikia hatua ya **uwiano ulio sawa.**

**Utekelezaji:** RAAWU itashawishi wadau wa maswala ya jinsia ili kuongeza ushiriki wa wanawake katika ngazi mbalimbali za Chama.

### 6.18 Haki za wanawake

- **Tamko:** RAAWU itahakikisha kuwa matamko yote ya kitaifa na kimataifa kuhusu haki za wanawake yanaheshimiwa na kuzingatiwa.

  **Mkakati:** RAAWU itahamasisha na kuelimisha wanawake kuhusu matamko ya haki za wanawake.

## 7.0 USIMAMIZI NA TATHMINI

Utekelezaji wa sera hii utategemea sana utashi wa kisiasa wa Chama (RAAWU), katika utambuzi na utoaji wa nyenzo muhimu za utekelezaji.

- Kamati za Wanawake katika ngazi zote, Tawi hadi Taifa, zitahusika moja kwa moja katika kuhakikisha kuwa malengo ya sera yanafikiwa.
- Ofisi ya Katibu Mkuu wa Chama, Kitengo cha Uratibu wa masuala ya jinsia itaandaa na kuwasilisha kwa Kamati ya Wanawake taarifa ya jumla ya maendeleo ya masuala ya jinsia katika Chama.
- Kamati za Wanawake katika ngazi zote, kwa kupitia vikao vyake vya kikatiba zitafanya tathmini kila baada ya miaka mitano (5) ya utekelezaji wa sera na kutoa maoni au mapendekezo yake katika vyombo husika vya Chama.